SHIRIKA LA MUNGU MWOKOZI
HALMASHAURI KUU YA SHIRIKA LA WASALVATORAIAN
Via della Conciliazione, 51
00193 ROMA (Italia)
Simu: +39 (06)68629.512; barua-pepe: milton.zonta@mailsds.org

Padre Milton Zonta
Mkuu wa Shirika

Itifaki AVB 20 – 052 SWA

Roma, 19 Machi 2020
Sherehe ya Mtakatifu Yosefu – Msimamizi wa Shirika

Kwenu nyote wanachama wa Shirika la Mungu Mwokozi

Ndugu wapendwa,

Ninawaandikia barua hii toka Nyumbamama yetu ambako tumetengwa tokana na Mlipuko wa COVID-19, maarufu unaojulikana kama Virusi vya Korona ambao umeendelea kusambaa duniani kote. Awali ya yote, ningependa nikushukuruni kwa salaam wa ukaribu wenu nasi katika siku hizi ngumu na za wasiwasi ambazo wengi wenu mmezielezea kama hali ya dharura, hasa hapa Italia, lakini kwa sasa katika Ulaya yote na sehemu zingine za dunia.

Hali hii mpya na isiyotegemewa inatulazimu si kubadili tu mipango yetu lakini pia kuhakiki hata taratibu zetu za kila siku, mathalan namna ya kusalimiana. Na zaidi ya hayo, kwa kulazimika kuingilia kati taratibu za mienendo yetu ya kila siku ya kimaisha hutufanya tutambue ni kwa namna gani tunaweza kupoteza upesi mambo ya msingi; hutufanya tuishi kwa hofu na kujiuliza kwa mapana juu ya matumaini na ujasiri wetu katika maisha.

Katika wakati huu mgumu wa majaribu, ningependa niwaalike kutafakari juu ya uwezekano wa kusoma maana ya nyakati hizi changamano. Kama Mwanzishi wetu alivyofanya wakati wake, ninawaalika kutambua maana ya "alama za nyakati" na kuendelea na njia yenu kwa kuhuisha matumaini katika maneno na ishara za Yesu Mwokozi wetu.

Bila ya kudunisha athari kubwa za janga hili katika maisha ya familia nyingi, ningependa niwaalike tuangalie mwelekeo wa misingi ambayo unaweza kutusaidia kutafakari kama mtu binafsi na kama jumuiya. Ninapendekeza zoezi la tafakari hii vilevile liangazwe kwa hekima ya kiroho ya Mwanzishi wetu Padre Fransis Yordan.

1. Bila ya kuwa tumepanga, hali hii ya dharura imetujia wakati maalum wa kipindi cha Kwaresma. Katika wakati huu, tunaitwa kuongoka na kujikania vitu vingi. *"Jenga nyumba ya utakatifu wako juu ya sala, kazi, unyamavu mkuu ..."* (SD II/8). Natumaini wakati huu wa unyamavu na jangwa utatusaidia kujiondoa katika ubinafsi wetu na kutuongoza katika zoezi halisi la maisha yetu ya sasa! Na tujiweke watupu nafsini ili tuweze kujazwa na Bwana, tukitumia muda mwingi katika sala pamoja naye, na wakati huo huo kumtambua Yesu katika nyuso za ndugu zetu ambao tunapaswa kuishi na kushirikishana nao muda huu muhimu tunaotengwa kwa lazima; na wakati huo huo tukimtambua Mwana wa Mungu katika uso mteswa wa wagonjwa wengi na katika vilio vya familia zao.

2. Bila ya kukusudia na kinyume kabisa na utashi wetu siku hizi zinatujia na uhalisia kuwa sisi sio wenye maweza yote. Kuna mipaka ambayo tunapaswa kuitambua na kuikubali. Sisi sio magangwe! Na wala hatukuitwa kufuata maisha ya mlengo wa kutoa vilivyo bora au upande wa wakamilifu ambako hakuna nafasi kwa yaliyo dhaifu au hatarini. *"Unyenyekevu, unyenyekevu, unyenyekevu. Oh, hazina kubwa kiasi gani!"* (SD III/11). Tunatumaini huu ni muda wa fasiri ya kujihurumia, kuwahudumia wazee miongoni mwa jamaa zetu na wanashirika wenzetu katika udhaifu wao, tukikumbatia vikomo na udhaifu wa kurithi kwenye maisha ya kila mmoja.

3. Hali hii imeamsha ufahamu juu ya umuhimu wa uhusiano wa kina na wa lazima kati yetu na wapendwa wetu. Nyakati hizi tunahisi thamani ya kutafuta mawasiliano na jamaa zetu kuliko nyakati nyingine zozote, hasa tukitaka kujua ni jinsi gani wanashirika na marafiki zetu wamejidhatiti katika kuchukua tahadhari. Kwa hiari kabisa, wasiwasi wa ndani na wa pamoja unakua katika moyo wa kila mmoja. *"Upole ni muhimu sana"* (SD II/66) kwa sababu katika hali kama hii ukuu wa ubinadamu ukaao ndani ya kila mmoja wetu hufunuliwa. Yawezekana si nyakati zote tunatambua ni jinsi gani ilivyo muhimu kuweka upole na ishara za upendevu kama kiini.

4. Shida hii ya kiafya imepelekea kuundwa kwa mitandao mbalimbali ya ushirikiano wa kijamii na ukarimu mkubwa miongoni mwa watu. Inafurahisha kusikia ushuhuda wa mshikamano na ishara za ujasiri katika vituo vya afya. Kwa kasi ya unajimu mitandao mingi ya kusaidiana na kushirikiana imeibuka kati ya watu wa pande zote. Mitandao hii ya mawasiliano kati ya watu hutufanya tutambue kuwa Mungu amepanda mioyoni mwetu misukumo ya asili katika kushirikiana, kupokeana na kushikamana. *"Watu wote na wakutumikie! Ndimi zote na zimsifu Bwana!"* (SD III/21)

5. Kwa kuangalia namna ambavyo virusi hivi vipya vinavyoenea kila mahali, tunatambua kwamba janga hili halina hisia za utaifa na wala halijui mipaka. Hakuna aliyesamehewa juu ya gonjwa hili pamoja na athari zake. Hakuna anayeweza kukwepa. Uhalisia huu mchungu umetengeneza vizuizi vya mgawanyiko na utengano kati yetu, na hata kusababisha hali ya kuogopana. *"Umaskini, mateso, dharau"* (SD IV/22). Tunatumaini uzoefu huu wa kutokuwa na ulinzi tena utatusaidia kuelewa vizuri hali ya ubaguzi na ukosefu wa usalama ambao watu wengi wamekuwa wakiishi tokana na sababu mbalimbali zisizo na idadi. Vile vile iwe mwaliko wa moja kwa moja wa kuchukua wajibu wetu na kujiuliza: tunawezaje kuwalinda watu wanaotuzunguka? Tunawezaje kuwapunguzia adha zao na kuwapelekea matumaini kidogo? Katika hali hii ukarimu ni kitu kisicho na gharama.

6. Moja ya makatazo ya muda mfupi ni pamoja na ya kutoadhimisha Ekaristi katika makanisa na uwepo wa jumuiya ya waamini ili kuepuka mikusanyiko na uwezekano wa maambukizi. Vyombo vya habari vinasaidia kwa kiasi fulani kuthibiti hali, vikifanya umoja wa kiroho uonekane kati ya wote katika kuumega Mkate. Hali hii hutupelekea kufikiri kwamba kutakuwa na maana gani kwa wengi kwamba Tridua ya Pasaka yawezekana isisherehekewe kiliturjia katika jumuiya? Vile vile, kuna maana gani ya kusherehekea Ufufuko wa Yesu katika ya hali ya wasiwasi na kifo? *"Katika Msalaba kuna wokovu, katika msalaba kuna uhai ..."* (SD I/189). Ni matumaini kwamba hali hii ambayo kamwe hatujawahi kuiona kabla, itatusaidia kusali kwa namna tofauti na kwa kina na haitaruhusu woga kupaza sauti dhidi ya matumaini katika mitazamo yetu. Na tutumie wasaa huu kuwa wakimya ili tuweze kusikiliza Mungu anataka kusema nasi nini katika nyakati hizi.

7. Haijalishi ni kwa namna gani hali ya utepetevu na kifo tunayoishi isivyoweza kuingiliana, tusipoteze nuru ya wito wetu katika kushirikishana vya kutosha juu ya uzima. *"Na uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe Mungu wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"* (SD I/83). Mungu tunayemjua na tunayemfanya ajulikane ni Mungu wa uzima na wa Ufufuko. Uhai tunaopokea toka kwa Mungu hauna mipaka, na wala kifo hakina sauti ya mwisho juu yake. Twatumaini hali hii itatuneemesha kwa kutuletea yaliyo bora ndani mwetu katika kuchangia na kushirikishana bila kuchoka mwelekeo wa maamuzi juu ya utume na uwepo wetu, isituruhusu kuwa wa kwanza kushindwa chini ya dola ya woga na kifo, ili tusiwe mashuhuda wa Ufufuko!

8. Katika dhana tofauti ya ulimwengu, tusishindwe na woga au kutokuwa na uhakika ni wapi hali hii inakojaribu kutupeleka. Huu ni wasaa wa kuungana na kuwa jirani na watu, hasa wanyonge, kuwasaidia kuishi hali hii isiyo ya kawaida toka matumaini ya kizio cha Mashariki. Zaidi ya hayo, ninakualika usijifungie mwenyewe badala yake kuwa mbunifu katika kutoa msaada wa kiroho ambao watu wanauhitaji sana toka kwetu. Asiwepo hata mmoja anatakayejisikia mpweke! Kwa hiyo basi tuendelee kuungana ... katika *"mwendelezo wa bidi ya sala na maombi"*, (SD II/14). Ulazima huo wa kujitenga hauwezi kuwa ishara ya wazi ya ubinafsi, bali yaweza kuwa ni nafasi maalum wa mwendelezo

wa neema tupewayo na Roho wa Kristo Mfufuka anayetualika katika ubunifu wa mapendo yanayoshinda vyote.

Ningependa kwa kumalizia kukumbushia wajibu wetu wa kufuata kanuni za afya za namna ya kujikinga kama zilivyoainishwa na Shirika la Afya Ulimwengu, maelekezo husika ya serikali mbalimbali, na vile vile miongozo ya kichungaji ya Kanisa mahalia katika nyakati hizi za changamoto. Muda huu na uwe wasaa wa kuongeza mapenzi yetu kwa Shirika na kutufanya kukua katika umoja kati yetu kwa njia ya sala, katika undugu na shughuli za kitume. Wote na tuhisi moyoni kuwa Padre Fransis Yordan anatusindikiza kwa mapendo yake kama baba na mlezi wa kiroho.

Kwa hiyo, na tusonge mbele tukiwa tumeungana katika sala na utume,

SOCIETATIS DIVINI SALVATORIS
SUPERIOR GENERALIS

Padre Milton Zonta SDS
Mkuu wa Shirika

Padre Agustin Van Baelen SDS
Katibu Mkuu